SOMO: KISWAHILI KATIKA SEKTA TOFAUTI ZA KAZI

SURA YA KWANZA : MAAMKIZI

1. DARASANI

Mwalimu: Habari za asubuhi?

Darasa: Nzuri;Shikamoo Mwalimu!

Mwalimu: Marahaba!

Mimi ni mwalimu.

Mimi ni nani ?

Kalisa: Wewe ni mwalimu.

Mwalimu: Vizuri !

Wewe Kayitesi ni mwanafunzi.

Kayitesi,wewe ni nani ?

Kayitesi: Mimi ni mwanafunzi.

Mwalimu: Ninyi wote ni wanafunzi.

Ninyi ni nani ?

Darasa: Sisi ni wanafunzi.

Mwalimu: Mimi sijambo !

Je,Musafiri hujambo ?

Musafiri: Sijambo mwalimu !

Mwalimu: Mimi mzima !

Je Kalisa wewe mzima ?

Kalisa: Mimi mzima !

Mwalimu: Ninyi wote wazima ?

Darasa: Sisi wote wazima !

Mwalimu: Vizuri!Kengele inalia kwa heri.

Darasa: Kwa heri mwalimu.

2. NYUMBANI

Kayitesi: Hodi!

Mama: Karibu!

Kayitesi: Shikamoo mama!

Mama: Marahaba!

Kayitesi: Pole kwa kazi mama !

Mama: Asante,habari za mchana ?

Kayitesi: Nzuri.

Mama: Habari za masomo Kalisa ?

Kalisa: Nzuri.

Mama na Kalisa: Nendeni,mweke vitabu,baada ya hapo mje hapa.

Kayitesi: Ndiyo mama.

Mama: Nendeni sokoni mkanunue vitunguu.

Kalisa na Kayitesi :Ndiyo mama !

Kalisa: Kwa heri mama !

Mama: Vizuri !Kwa heri.

SURA YA PILI: NAFSI

I. MAZUNGUMZO

Mwalimu :Habari za mchana ?

Darasa :Nzuri shikamoo mwalimu !

Mwalimu :Marahaba !Kalisa mimi ni nani ?

Kalisa :Wewe ni mwalimu.

Mwalimu :Vizuri,mimi ni mwalimu.Habimana wewe ni nani ?

Habimana :Mimi ni mwanafunzi .

Mwalimu :Vizuri ! Darasa ,nyinyi ni nani ?

Darasa :Sisi ni wanafunzi.

Mwalimu :Vizuri .Habimana,Umutesi pia ni nani ?

Habimana :Umutesi,yeye pia ni mwanafunzi.

Mwalimu :Umutesi na Nyirimana wao ni nani ?

Kalisa : Umutesi na Nyirimana wao pia ni wanafunzi.

TAZAMA :

Umoja :	**Wingi :**
Mimi	**Sisi**
Mimi ni mwalimu	**Sisi** ni wanafunzi.
Yeye	**Wao**
Yeye ni mwanafunzi	**Wao** ni wanafunzi

Wewe **Ninyi/nyinyi/nyie**

Wewe ni mwalimu **Ninyi** ni walimu.

II. KIFUNGU CHA KUSOMA.

(i) **Mimi** ninacheza mpira. mimi na kalisa tunacheza mpira. **Sisi** tunacheza mpira. **Wewe** unacheza mpira pia. Wewe na Gatabazi mnacheza mpira. **Ninyi** mnacheza mpira pia. Yeye anacheza mpira. **Yeye** na Musafiri wanacheza mpira pia. **Wao** wanacheza mpira.

(ii) **Yeye** anapika chakula. **Wewe** unafagia. **Sisi** tunasoma Kiswahili. **Wao** wanachota maji. **Nyie** mnaimba. **Mimi** nawatazama.

Kwa mfano:

Umoja: Wewe **na mimi** tunasoma. Wewe **nami** tunasoma.

Wingi: Ninyi **na** sisi tunasoma.**Ninyi nasi** tunasoma.

Umoja: Yeye **na wewe** mnasoma. **Yeye nawe** mnasoma.

Wingi: wao **na ninyi** mnasoma. **Wao nanyi** mnasoma.

Umoja: mimi **na yeye** tunasoma. **Mimi naye** tunasoma.

Wingi: Sisi **na wao** tunasoma. **Sisi nao** tunasoma.

ZOEZI

A. Jaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kutumia nafsi inayofaa.

1. _____ ninaandika daftarini.
2. _____ Wanajifunza Kiswahili.
3. _____ mnafanya nini?
4. _____ tunasoma na_____mnacheza.
5. _____ unamenya ndizi.

B. Andika sentensi zifuatazo katika umoja au wingi.

1. Mimi na yeye tunalima.
2. Wewe unatoka Kigali.
3. Sisi tunaondoka sasa hivi.
4. Wao wansali.
5. Ninyi mnapenda kazi.

SURA YA TATU: HESABU

Sehemu za hesabu:

1. Kuhesabu
2. Sehemu
3. Desimali
4. Saa
5. Nyakati za Siku

A. Kuhesabu

Mia moja na saba (107)

Mia mbili thelathini na tatu (233)

Elfu moja (1,000)

Elfu nane na nane (8, 008)

Elfu tatu mia tano ishirini na moja (3,521)

Laki moja (100,000)

Laki nne hamsini na sita elfu mia tano na tatu (456, 503)

Milioni moja (1,000,000)

Miliono mbili, laki tatu na tisisni na nne elfu mia tano na thelathini na nne (2,394,538)

Biliono moja (1,000,000,000)

B. Sehemu

1/2 : Nusu

1/3 : Theluthi

¼ : Robo

1/5 : Moja kwa tano/ moja juu ya tano

1/6 : Sudusi

1/7 : Moja kwa saba/ moja juu ya saba

1/8 : Moja kwa nane/ moja juu ya nane

1/9 : Moja kwa tisa

1/10 : Moja kwa kumi

2/3 : Theluthi mbili

¾ : Robo tatu

C. DESIMALI

1.1 : Moja nukta moja (moja desimali moja)

1.25 : Moja nukta mbili tano

1.534 : Moja nukta tano tatu nne

204.3 : Mia mbili nne na nukta tatu

D. Saa

Saa 12 : 00 kumi na mbili kamili

Saa 12 : 10 kumi na mbili dakika kumi

Saa 12 : 30 kumi na mbili na nusu/ saa kumi na mbili na dakika thelathini

Saa 6 : 00 sita kamili mchana(adhuhuri)

E. NYAKATI ZA SIKU

Siku moja inaweza kugawanywa katika nyakati kuu zifuatazo :

Alfajiri : Wakati kunapo karibia kupambazuka

Asubuhi : Tokea kucomoza jua hadi likiwa utosini

Adhuhuri : Wakati jua linapo kuwa utosini

Alasiri : Kati ya saa tisa na saa kumi na nusu za mchana

Magharibi : Kuanzia jua linapokaribia kuzama hadi kupotea kwa nuru yake

Usiku : Kuanzia magharibi iishapo hadi asubuhi

Usiku wa manane : Katikati ya usiku

F. MWAKA

(1) Mwaka moja una siku mia tatu na sitini tano au siku mia tatu sitini na sita ifikapo mwaka mkubwa.

(2) Mwaka moja una miezi kumi na miwili.
Miezi hiyo ni:

1. Januari
2. Februari
3. Machi
4. Aprili
5. Mei
6. Juni
7. Julai
8. Agosti
9. Septemba
10. Oktoba
11. Novemba

12. Desemba

Mwaka moja una majuma au wiki **hamsini na mbili**.

Siku za wiki ni :

1. Jumamosi
2. Jumapili
3. Jumatatu
4. Jumanne
5. Jumatano
6. Alhamisi
7. Ijumaa

SURA YA NNE: MATUMIZI YA NYAKATI

1. WAKATI ULIOPO (-na-)

Tungo yakinishi :	**Tungo kanushi :**
Umoja: Mimi ni**na**lima shambani.	Mimi **si**limi shambani.
Wewe u**na**lima shambani.	Wewe **hu**limi shambani.
Yeye a**na**lima shambani	yeye **ha**limi shambani
Wingi: Sisi tu**na**lima shambani	Sisi **ha**tulimi shambani
Ninyi m**na**lima shambani	Ninyi **ha**mlimi shambani
Wawo wa**na**lima shambani	Wawo **ha**walimi shambani

2. WAKATI UJAO (-ta-)

Tungo yakinishi	**Tungo kanushi**
Umoja: Mimi ni**ta**enda marekani	Mimi **si**taenda marekani

Wewe u**ta**enda marekani	Wewe **hu**taenda marekani
Yeye a**ta**enda marekani	Yeye **ha**taenda marekani
Wingi: Sisi tu**ta**enda marekani	Sisi **ha**tutaenda marekani
Ninyi m**ta**enda marekani	Ninyi **ha**mtaenda marekani
Wawo wa**ta**enda marekani	Wawo **ha**wataenda marekani

2. WAKATI ULIOPITA(-LI-)

Tungo yakinishi	**Tungo kanushi**
Umoja : Mimi ni**li**muona shuleni	Mimi si**ku**muona shuleni
Wewe u**li**muona shuleni	Wewe hu**ku**muona shuleni
Yeye a**li**muona shuleni	Yeye ha**ku**muona shuleni
Wingi: Sisi tu**li**muona shuleni	Sisi hatu**ku**muona shuleni
Ninyi m**li**muoana shuleni	Ninyi ham**ku**muona shuleni
Wawo wa**li**muona shuleni	Wawo hawa**ku**muona shuleni

3. WAKATI WA MAZOEA (-hu-)

Tungo yakinishi	**Tungo kanushi**
UMOJA:	
Mimi **hu**lima shamba	Mimi **si**limi shamba
Wewe **hu**la nyama	Wewe **hu**li nyama.
Yeye **hu**shona nguo.	Yeye **ha**shoni nguo
WINGI:	
Sisi **hu**lima shamba	Sisi **ha**tulimi shamba.

Nyinyi **hu**la nyama.	Nyinyi **ha**mli nyama.
Wao **hu**shona nguo.	Wao **ha**washoni nguo

5. WAKATI ULIOTIMILIKA (-me-)

Tungo yakinishi	**Tungo kaanushi**
Umoja: Mimi ni**me**kula andazi	Mimi si**ja**kula andazi
Wewe u**me**kula andazi	Wewe hu**ja**kula andazi
Yeye a**me**kula andazi	Yeye ha**ja**kula andazi
Wingi: Sisi tu**me**kula andazi	Sisi hatu**ja**kula andazi
Ninyi m**me**kula andazi	Ninyi ham**ja**kula andazi
Wawo wa**me**kula andazi	Wao hawa**ja**kula andazi

SURA YA TANO: MSAMIATI –UHUSIANO WA FAMILIA

1. UHUSIANO WA MUME,MKE NA WATOTO NA NDUGU WA UPANDE WA MUME

- Mtoto
- Mume
- Mke
- Mwanamume
- Mwanamke
- Kaka
- Dada
- Baba
- Mama
- Babu
- Bibi au nyanya.
- Mjukuu
- Baba mdogo
- Mama mdogo
- Shangazi
- Binamu

3. UHUSIANO WA MUME,MKE,WATOTO NA NDUGU WA UPANDE WA MKE

- Baba mkwe
- Mama mkwe
- Wajukuu
- Shemeji
- Mjomba
- Wapwa

SURA YA SITA: VIUNGANISHI NA VIHUSISHI

1. VIUNGANISHI

- Na
- Au
- Wala
- Pia
- Vilevile
- Pamoja na
- Kisha
- Baadaye
- Halafu
- Hata
- Kwa sababu
- Ili
- Ila
- Lakini
- Isipokuwa
- Kama
- Kuwa
- Kwamba
- Madhali

2. VIHUSISHI

- Ya
- Kwa
- Chini ya
- Juu ya
- Nyuma ya
- Mbele ya
- Nje ya
- Ndani ya
- Kabla ya
- Baada ya
- Kati ya
- Katika
- Katikati ya
- Pembeni mwa
- Mbali na
- Bila ya
- Kwa sababu ya
- Kwa ajili ya
- Kutoka kwa